HOTUBA YA ND. WELLINGTON CHIBEBE, MKURUGENZI WA SHIRIKA LA KAZI DUNIANI (ILO) KWA NCHI ZA

TANZANIA, KENYA, RWANDA, BURUNDI NA UGANDA

SIKU YA AFYA NA USALAMA KAZINI

JUMAMOSI, APRILI 28, 2018

VIWANJA VYA KICHANGANI, IRINGA, TANZANIA.

Mh. Jenista Mhagama (Mb) –Waziri wa nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge, kazi, ajira, vijana na wenye ulemavu.

Mh. Antony Mavunde (Mb)–Naibu Waziri kazi ajira na watu wenye ulemavu

Nd. Eric Shitindi Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, ajira, shughuli za bunge, vijana na watu wenye ulemavu.

Mama Amina Juma Masenza – Mkuu wa mkoa wa Iringa.

Mama Hadija Mwenda-Mtendaji Mkuu, OSHA

Dr Aggrey Mlimuka, -Mkurugenzi Mtendaji , ATE

Dr. Yahya K. Msigwa, Katibu Mkuu, TUCTA

Washiriki na wafanyakazi.

Waandishi wa habari,

Itifaki imezingatiwa,

Nd. Mgeni Rasmi na wageni waalikwa

Kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Kazi Duniani **(ILO)** Nd. Guy Ryder, Mkurugenzi wa Kanda ya Afrika, Mama Cynthia Samwel - Olonjuwon na kwa niaba yangu mimi mwenyewe, nawaletea salamu kutoka Shirika la Kazi Duniani tunapoadhimisha

siku hii muhimu ya Afya na usalama kazini tukiwa na kauli mbiu isemayo "Kizazi salama chenye Afya kwa uchumi na maendeleo ya Viwanda." Ni siku ambayo serikali, waajiri na wafanya kazi ulimwenguni kote hujikumbusha kuzuia magonjwa na ajali mahala pa kazi na kuhakikisha kuwa usalama na Afya kazini ni mojawapo ya nguzo muhimu katika lengo zima la kuendeleza kazi zenye staha.

Tukumbuke kuwa kiasi cha wafanyakazi milioni 2.78 ulimwenguni wanafariki kila mwaka kutokana na kuumia au magonjwa kazini wengi wao (milioni 2.4) ikiwa ni kutokana na magonjwa kazini. Idadi hii ya watu kupoteza maisha haikubaliki na inaweza kuzuilika. Tuungane pamoja kuleta mabadiliko.

Mwaka huu, kauli mbiu yetu inaweka msisitizo kuboresha Afya na usalama kazini kwa vijana walio makazini na hasa kupambana na utumikishwaji wa watoto. Kampeni hii inalenga kuboresha utekelezaji wa malengo ya maendeleo endelevu ya Dunia **(SDGs)** hasa Na. 8 - Kipengele Na 8.8 kinachohusu kuwa na mazingira salama kwa wafanya kazi na pia Na. 8.7 kinachohusu kukomesha utumikishaji wa watoto ifikapo mwaka 2025. Kauli mbiu hii inatuhimiza pia kuwepo ajira zenye staha kwa vijana.

Ili kufanikisha haya tunahitaji juhudi za pekee za pamoja.

Nd. Mgeni Rasmi na wageni waalikwa

Vijana wengi ulimwenguni kote wanafanya kazi kwa masaa mengi hasa kwenye sekta isiyo rasmi, kwenye makubaliano yenye utata na mazingira yasiyo salama. Kwenye nchi zinazoendelea vijana ndio sehemu kubwa ya wale wasio na ajira, wale walio kwenye sekta isiyo rasmi, maeneo ya mijini na vijijini.

Kuwaacha vijana wakiwa wadogo kwenye kazi hatarishi husababisha madhara mbalimbali yanayo mkwaza kijana kufanikiwa kwenye ajira zenye staha kwa maisha yake ya baadaye. Madhara haya yanaweza kuwa ya kielimu, kimwili, kisaikolojia na kijamii.

Kwa Tanzania, kotokana na utafiti wa nguvukazi wa **2014 (ILFS),** vijana wa umri miaka 15-35 wanaofanya kazi ni theluthi moja ya idadi ya wafanyakazi wote na asilimia 82 ya vijana hao wapo kwenye ajira zisizokuwa rasmi.

Nd. Mgeni Rasmi na wageni waalikwa

Vijana ulimwenguni

- Kiwango cha ukosefu wa ajira kwa vijana ulimwenguni (2017) kinakadiriwa kuwa 13.1% na vijana wapatao million 70.9 hawana ajira ukilinganisha na million 76.7

mwaka 2009, kipindi cha mgogoro wa kiuchumi. Hapa Tanzania kiwango cha ukosefu wa ajira ni 10.3% ukilinganisha na kile cha vijana 11.7%. **(Taarifa ya utafiti wa Nguvukazi - ILFS 2014**)

- Vijana wafanyakazi wapatao mil.541 (miaka 15- 24), wakiwemo watoto mil. 37 wanaofanya kazi kwenye mazingira hatarishi, ni zaidi ya 15% ya nguvu kazi yote ulimwenguni. Inakadiriwa kuwa vijana hawa hupata ajali kazini kwa zaidi ya asilimia 40 ikilinganishwa na wale wenye umri zaidi ya miaka 25.
- Ulimwenguni kote, vijana watatu kati ya wanne (3/4) walioajiriwa wapo kwenye ajira zisizo rasmi ukilinganisha na idadi ya watatu kati ya watano (3/5) ya watu wazima. **(ILO WESO 2018).**

Hali hizi za vijana ni lazima ziangaliwe na kuona jinsi ya kuziboresha ili ziwe kwenye hali zinazokubalika. Hii ni kazi yetu wote – Serikali, waajiri, wafanyakazi na vijana wenyewe.

Zipo sababu nyingi zinazo weza kuwafanya vijana kuwa kwenye mazingira ya kazi hatarishi k.m. hatua za kukua kwao kimwili na kisaikolojia, kuwepo vitendea kazi hatarishi na kushindwa kufanya makubaliano sahihi hasa kwa kazi za hatari au zilizo kwenye mazingira hatarishi.

Nd. Mgeni Rasmi na wageni waalikwa

Vihatarishi mbalimbali vinavyoweza kuwepo sehemu za kazi zinazoweza kuathiri usalama na afya kwa vijana mahala pa kazi - ni pamoja na - kufanya kazi kwenye maeneo ya juu, kutumia mitambo au vifaa ambavyo ni vya hatari, kutumia vifaa au madawa yanayo lipuka, chini ya maji, chini ya ardhi, kutumia madawa au kemikali za sumu k.m. kwenye kilimo. n.k.

Zifuatazo ni baadhi ya hatua zinazoweza kuchukuliwa ili kuboresha hali ya usalama na afya kazini kwa vijana:

- "Kazi salama huashiria kazi zenye staha". Waajiri wahakikishe kuwa maeneo ya kazi, mitambo, mashine n.k. Vipo salama kwa wafanyakazi na hasa vijana.
- Wafanyakazi, wakiwemo vijana, wazifahamu na kuzitekeleza sheria na kanuni zinazolenga kupunguza viwango vya ajali na matatizo ya kiafya kazini.
- Utafiti ufanywe ili kufahamu idadi ya vijana walio kwenye mazingira ya kazi hatarishi. - kama kwenye sekta isiyo rasmi, mazingira ya nyumbani na kwenye mashamba. K.m. Barani Afrika 83% ya watoto wanaofanya kazi wapo kwenye sekta ya kilimo, ukilinganisha na hapa Tanzania kiasi cha watoto mil. 4.2 (miaka 5-17) wapo kwenye utumikishwaji, 92% wapo kwenye sekta ya kilimo, uvuvi na misitu.

Tunapongeza juhudi za serikali na wadau wengine katika kupambana na janga la utumikishwaji wa watoto kwenye sekta mbalimbali, ikiwemo ya kuboresha mpango kazi wa kitaifa wa kupambana na utumikishwaji wa watoto. **(NAP).**

- Usajili wa maeneo ya kazi na ukusanyaji wa taarifa kuhusu afya na usalama kazini kama zoezi endelevu, linaloendelea kwa sasa na OSHA, na kuainisha kazi hatarishi hasa kwa vijana, itasaidia utambuzi wa kuwepo hali za hatari kazini, sekta hatarishi, vikundi vilivyo kwenye hali hatarishi na kuona hatua mbalimbali za kuchukua ili kuwaokoa vijana kwenye hali hiyo.
- Kuendesha kampeni zinazohusu kuboresha ufahamu wa vijana kuhusu afya na usalama kazini na pia kujumuisha maswala haya kwenye mitaala ya elimu kutasaidia makundi hayo kufahamu kuhusu kanuni, sheria n.k. na maeneo ya kutoa kipaumbele kwa vijana. Kwa mfano mwaka huu OSHA imedhamiria kufikia zaidi ya vijana 5000. Eneo hili linaimarishwa kwa kuwepo sera ya Afya na usalama kazini ya mwaka 2010, ambayo ipo kwenye marekebisho. Sera inawatambua pia vijana kama kundi mojawapo lililo kwenye hali hatarishi, pia inasisitiza kuwepo kwa programu za uhamasishaji kwenye sekta isiyo rasmi.

Nd. Mgeni Rasmi na wageni waalikwa

Tunaipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, chini ya uongozi thabiti wa Mh. Dr. John Pombe Magufuli sio tu katika ushiriki wake kikamilifu katika kuandaa mikataba ya kazi ya kimataifa bali pia katika kuwa mstari wa mbele katika kuridhia na utekelezaji wa mikataba hiyo. Tunatambua juhudi zinazoendelea kufanyika katika kuridhia mikataba na 155, 161, 167, 184 na 187 ambayo ni muhimu katika kufanya sehemu za kazi kuwa salama zaidi.

Kuanzishwa kwa mfuko wa fidia wa wafanyakazi **(WCF)** mwaka 2015 chini ya sheria ya mwaka 2008 ni hatua nzuri ya kuondoa migogoro inayohusu fidia kwa wafanyakazi kutokana na vifo au ajali kazini: kwa sasa taarifa zinasema kuwa zaidi ya 2.52bn/= zimeshalipwa kwa wafanyakazi.

Mpango wa pili wa maendeleo wa miaka 5 (2016/17 – 2020/21 unaolenga maboresho ya maendeleo ya uchumi na kuelekea kwenye uchumi wa viwanda ni nguzo kuu ya kufikia malengo ya dira ya 2025 na pia kuifikisha Tanzania kuwa kati ya nchi za uchumi wa kati. Inafurahisha kuona kuwa maendeleo ya vijana ni mojawapo ya vipaumbele kwenye utekelezaji wa mpango huu.

Juhudi zote hizi zitasaidia sana katika kuboresha utekelezaji wa maswala ya afya na usalama kazini kitaifa na pia kusaidia kuleta maendeleo kwenye sekta mbalimbali za

uchumi. Kwani lengo la kuboresha hali ya usalama na afya kazini kwa vijana linaweza kufikiwa tu kwa kujumuisha juhudi kutoka kwa wadau/watendaji mbalimbali .

Napenda kuwahakikishia ushirikiano wa karibu wa Shirika la Kazi Duniani (ILO) katika kujumuisha mikataba ya kimataifa ya kazi (International Labour Standards) kwenye mipango mbalimbali ya afya na usalama kazini.

Tuungane katika kuboresha utamaduni wa afya na usalama kazini kwa wafanyakazi vijana, wafanyakazi wote ili kuokoa maisha na kukomesha utumikishwaji wa watoto.

Nawatakia siku njema ya afya na usalama kazini -2018

Asanteni kwa kunisikiliza.